

- Kuwa mfano wa kuigwa, kwa kushirikiana na mwenza wake katika afya ya uzazi
- Kufanya jitihada ya kupata taarifa sahihi kuhusu afya ya uzazi na uzazi wa mpango
- Kujadiliana na mwenza kuchagua njia ya uzazi wa mpango inayowafaa
- Kutumia njia za uzazi wa mpango maalumu kwa wanaume yaani kondomu au kufunga uzazi
- Kujadiliana na mwenza jinsi ya kukabiliana na changamoto au maudhi madogo madogo ya uzazi wa mpango na kutafuta ushauri wa kitaalamu
- Kujadili na wanaume wenzake kuhusu swala la afya ya uzazi na uzazi wa mpango
- Kuwahi kituo cha kutolea huduma za afya kwa ajili ya uchunguzi na ushauri wa matatizo yoyote ya afya ya uzazi mfano; magonjwa ya kujamiiana VVU/UKIMWI na ugumba/utasa.
- Kutoa msaada wa hali na mali kwa mama mjamzito na mtoto pale inapotakiwa
- Kuacha na kukemea ukatili dhidi ya wana wake na watoto

KUMBUKA

**“Mwanaume wa mfano
hushirikiana na mwenza wake”**



Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii,
Jinsia, Wazee na Watoto

USHIRIKI WA WANAUME KATIKA HUDUMA ZA AFYA YA UZAZI



**Mwanaume wa Kuigwa
ni yule anayeshirikiana na mwenzi wake**



Ushiriki wa Wanaume Katika Huduma za Afya ya uzazi

Kwa nini ushiriki wa wanaume ni muhimu?

Swala la kupata mtoto linahusisha watu wawili mwanamke na mwanaume au kijana wa kiume na wa kike. Hata hivyo wanaume wamekuwa hawashiriki kikamilifu katika afya ya uzazi kwa sababu mbalimbali zikiwemo:

- Mfumo dume
- Mila na desturi
- Kutokujali
- Kutokuwa na uelewa
- Kwa muda mrefu, mfumo wa utoaji wa huduma za afya ya uzazi ulilenga wanawake

Kuna umuhimu gani wa ushiriki wa wanaume katika afya ya uzazi?

- Wanaume kama wanawake wana haki ya kupata taarifa na huduma za afya za uzazi
- Wenzi kwa pamoja wana wajibu wa kujikinga na mimba zisizotarajiwa na maambukizi ya VVU
- Baadhi ya njia za uzazi wa mpango huhitaji uamuzi wa pamoja

- Baadhi ya wanaume wana uelewa mdogo kuhusu uzazi wa mpango
- Wanaume wengi wana dhana potofu kuhusu njia za uzazi wa mpango na hivyo kuwa kikwazo katika matumizi ya njia hizi
- Baadhi ya wanaume hufikiri kutumia uzazi wa mpango hupelekea mwanamke kuwa na wanaume wengi
- Ushiriki wa wanaume huimarisha mawasiliano baina ya wenza
- Ushiriki wa wanaume husaidia kutambua majukumu yao katika malezi ya watoto
- Ushiriki wa wanaume husaidia kutambua kwamba si wanawake tu bali hata wanaume wanaweza kukosa uzazi (ugumba)

Ni madhara gani yatokanayo na ushiriki mdogo wa wanaume?

- Kukosa uaminifu baina ya wenza
- Matumizi madogo au matumizi yasiyo sahihi ya uzazi wa mpango
- Ukatili wa kijinsia mfano kupiga mwanamke baada ya kugundua anatomia uzazi wa mpango
- Kutumia uzazi wa mpango kwa kificho kwa kuogopa kupigwa
- Kukosa mawasilano baina ya wenza na hivyo

kusababisha mimba zisizotarajiwa

- Utoaji wa mimba kwa njia zisizo salama
- Maambukizi ya VVU na magonjwa ya kujamiiana
- Mfarakano wa familia baada ya mmoja wapo kugundulika ana VVU
- Ongezeko la watoto wa mitaani au kutupa watoto na malezi ya mzazi mmoja
- Msongo wa mawazo

Jinsi wanaume wanavyoweza kushiriki katika afya ya uzazi

- Kwenda na mwenzi wake kituo cha huduma za afya wakati wa ujauzito, kujifungua au kupeleleka mtoto kliniki

